

Ameniwaka huru kweli
(Il m'a vraiment libéré/ He really set me free)

Ameniwaka huru kweli, naimba sasa: Haleluya!
Kwa msalaba nimepata kutoka katika utumwa.

Nimeokoka, nafurahi! Na dhambi zangu zimetoka.
Nataka kumtumikia Mwokozi wangu siku zote.

Zamani nilifungwa sana kwa minyororo ya shetani,
nikamwendea Bwana Yesu, akaniweka huru kweli.

Nimeokoka, nafurahi! Na dhambi zangu zimetoka.
Nataka kumtumikia Mwokozi wangu siku zote.

Neema kubwa nilipata kuacha njia ya mauti,
na nguvu ya wokovu huo yanichukua siku zote.

Nimeokoka, nafurahi! Na dhambi zangu zimetoka.
Nataka kumtumikia Mwokozi wangu siku zote.

Na siku moja nitafika mbinguni kwake Mungu wangu.
Milele nitamhimidi na kumwimbia kwa shukrani.

Nimeokoka, nafurahi! Na dhambi zangu zimetoka.
Nataka kumtumikia Mwokozi wangu siku zote.

Mwokozi wangu ni mwamba bora

1

Mwokozi wangu ni mwamba bora, ahadi kama milima;
zaniletea amani tele, na mibaraka daima.

Katika mwamba ni raha kuu, baraka tele kutoka juu.

Nakaa humo, ninastarehe, ni heri sana milele.

2

Makimbilio ni mwamba huo katika teso lo lote;

Nisikimbie adui 'kuu, nishinde katika vyote!

Dunia yote ikitingika, ahadi zake hazipunguki.

Nakaa humo, ninastarehe, ni heri sana milele.

3

Nakaa mbali ya udhalimu, hatia, dhambi, hukumu.

Na kwa imani nikisimama, adui atakimbia.

Nayo mawazo ya giza tupu hayatapata nafasi huko.

Nakaa humo, ninastarehe, ni heri sana milele.

4

Nafurahia baraka zote za ulimwengu wa roho.

Karama hizo nalizipewa katika kufa kwa Yesu.

Hakuna woga na shaka huko, hayatakuwa manung'uniko.

Nakaa humo, ninastarehe, ni heri sana milele.